



TAARIFA KWA UMMA

SHINDANO LA KUBUNI NEMBO YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA

UTANGULIZI

Wakala wa Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) ulianzishwa Mwaka 1999 kwa lengo la kuendesha, kusimamia, kuboresha na kuendeleza Viwanja vya Ndege vinavyomilikiwa na Serikali Tanzania Bara.

MAJUKUMU YETU

- i. Kuendesha, kusimamia, kuboresha na kuendeleza viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali kwa utaalamu na ghamama nafuu;
- ii. Kutoa huduma bora zenye ufanisi na salama pamoja na vifaa wezeshi kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege ili kujenga taswira nzuri ya nchi kwa mataifa mengine duniani;
- iii. Kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa Serikali kuhusu uendelezaji wa viwanja vya ndege;
- iv. Kuhakikisha kwamba sera ya Serikali kuhusu viwanja vya ndege, kanuni na taratibu zinatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa;
- v. Kuishauri Serikali katika masuala ya Kitaifa na Kimataifa yanayohusu masuala ya usimamizi wa viwanja vya ndege, kanuni, ada na tozo; na
- vi. Kuchangia maendeleo ya uchumi wa nchi kwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu muhimu, vifaa wezeshi na huduma katika viwanja vya ndege.

DIRA

Kuwa mtoaji bora wa huduma za uendeshaji viwanja vya ndege Duniani.

DHIMA

Kutoa huduma bora na viwezeshi katika Viwanja vya Ndege kwa kuzingatia Usalama na Ufanisi kwa wadau wa Viwanja vya Ndege kwa lengo la kukuza Uchumi na maendeleo ya jamii.

VIGEZO VYA KUZINGATIA KATIKA UBUNIFU NEMBO

TAA inakusudia kutengeneza nembo mpya ambayo itaakisi Dira, Dhamira na majukumu yake. Kwa ajili hiyo, wabunifu wanaalikwa kushiriki katika shindano la kuunda nembo mpya ya TAA ambayo itaeleza kwa upekee na kwa uwazi juu ya TAA, kazi zake na kauli mbiu yake (**TAA Inaunganisha Tanzania na Dunia**). Vijana na makampuni binafsi wanahimizwa kushiriki.

SIFA ZA KINA ZA SHINDANO

Nembo inayobuniwa ni lazima iwe na sifa zifuatazo:

- i. Itafsiri majukumu, dira na dhima ya TAA.
- ii. Iwe na rangi ya kijani, manjano, bluu, na rangi nyeusi zenye mwonekano wa hali ya juu
- iii. Isifanane na nembo iliyokuwepo hapo awali
- iv. lambatane na maelezo ya kimaandishi ya maana na vipengele vyake.
- v. Ikiwa nembo inajumuisha maandishi, mshiriki lazima aweze kutoa jina la aina ya maandishi hayo.
- vi. Nembo inapaswa kuwa katika mfumo wa aina mbili za faili za JPEG na PNG
- vii. TAA itahifadhi haki ya kusajili nembo itakayochaguliwa kama alama yake ya huduma
- viii. Uamuzi wa TAA juu ya uchaguzi wa Nembo inayofaa utakuwa wa mwisho na hautakuwa wazi kwa rufaa yoyote.
- ix. TAA itawasilisana na Mbunifu husika kwa ajili ya kuwasilisha muundo wake au kupata maelezo zaidi ya ufanuzi.


TUZO YA MSHINDI

Mshindi wa shindano la ubunifu wa nembo mpya ya TAA atapatiwa zawadi ya fedha taslimu kiasi cha Shilingi Milioni Moja za Kitanzania (1,000,000/=) baada ya TAA kuridhika na uthibitisho juu ya ubunifu wa nembo husika.

Wafanyakazi wa TAA hawastahili kushiriki shindano hili.

TARATIBU ZA UWASILISHAJI

Nembo hiyo iwasilishwe kwa (nakala laini) pamoja na maelezo ya mawasiliano ya mbunifu kwa Mkurugenzi Mkuu wa TAA kupitia barua pepe ya info@airports.go.tz kabla au ifikapo tarehe 18/09/2022.


Mussa I. Mbura

MKURUGENZI MKUU

AMINO
VIEDEO VYA LITAFADHILA KATANZANIA

"Inaunganisha Tanzania na Dunia"

Mawasiliano yote yapelekwe kwa MKURUGENZI MKUU

Anuani: 1206 Mtaa wa Kinawa, S/L R. 18000 Dar es Salaam, Tanzania. Sifuri: +255 22 221 1001. Mwaka: 2022